



MARUDIO YA TANGAZO

TANGAZO LA KUPOKEA MAOMBI YA LESENI KWA KAMPUNI ZA UKUSANYAJI NA UGAWAJI WA MIRABAHA (COLLECTIVE MANAGEMENT ORGANIZATIONS – CMOs) TANZANIA BARA KATIKA DARAJA LA KAZI ZA MAANDISHI, FILAMU, SANAA ZA UFUNDI NA SANAA ZA MAONESHU.

Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999 kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Fedha Na. 5 ya mwaka 2022 iliruhusu uanzishwaji wa Makampuni binafsi yatakayokuwa na jukumu la kukusanya na kugawa Mirabaha kwa pamoja yaani *Collective Management Organizations (CMOs)*.

Ofisi inapenda kukaribisha Kampuni yoyote yenye nia ya kupatiwa Leseni ili kufanya kazi kama CMOs Tanzania Bara katika daraja la Kazi za Maandishi, Filamu, Sanaa za Ufundi na Sanaa za Maonesho kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kuwasilisha maombi rasmi kwa kuzingatia vigezo vinavyopatikana katika Kanuni za Hakimiliki na Hakishiriki (Kampuni za Ukusanyaji na Ugawaji wa Mirabaha) 2023, Toleo Namba 215 na 211 la tarehe 24 Machi, 2023. Kanuni hizi pia zinapatikana katika tovuti ya Ofisi: www.cosota.go.tz

Masharti ya kupatiwa leseni kwa Kampuni ni kama ifuatavyo;

1. Iwe inamilikiwa na Watanzania (iwasilishe vitambulisho vya wamiliki wa Kampuni – Mf. NIDA, Hati ya kusafiria).
2. Nakala za picha za wamiliki (passport size).
3. Iwe na Hati ya namba ya mlipakodi (TIN) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania.
4. Iwe na hati ya mlipa kodi (Tax clearance certificate) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).
5. Iwe na Leseni ya biashara kutoka Mamlaka husika.
6. Iwe na cheti cha usajili wa jina la kampuni kutoka BRELA.
7. Iwe na Hati ya usajili wa makampuni (Certificate of incorporation).
8. Iwe na *Memorandum and Article of Association*.
9. Iwe na wasifu wa wamiliki.
10. Iwasilishe dhamana ya utendaji (Performance Bond/Collateral) yenye thamani isiyopungua milioni mia mbili hamsini.
11. Iwasilishe mpango kazi wa namna ambavyo Kampuni itakusanya na kugawa mirabaha kwa ufanisi.
12. Iwasilishe orodha ya uthibitisho wa Wanachama wasiopungua thelathini ambao inatarajia kuwawakilisha (majina, namba za simu na salni zao).
13. Iwe haijawahi kupatikana na hatia ya ukwepaji kodi au uhujumu uchumi.
14. Kufuata Sheria na kanuni zote za Nchi. (Namba 13 na 14 - Kampuni iwasilishe kiapo kutoka kwa Mwanasheria)

Tafadhali tambua kuwa: Maombi ya Leseni yatapokelewa ndani ya siku 30 kuanzia tarehe 22 Juni, 2023 ya tangazo hili na maombi yawasilishwe kupitia anuani ifuatayo:

Katibu,
Bodi ya Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA),
S.L.P 6388,
Dar es Salaam.
Tafadhali andika neno "CMO" juu ya bahasha.

HABARILEO
UK 5

22/06/2023

Imetolewa na;
Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA),
S.L.P 6388, Dar es salaam.
SIMU: 0738 015013